OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MBINGA MWAKA 2021

SHULE YA SEKONDARI NGWILIZI

S.L.P 152,

MBINGA.

SIMU NA. **+255752078 280/0625298 657.**

+255766172 375/0627139 151

MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGWILIZI HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA MWAKA 2021.

UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha.....katika shule hii mwaka 2021 baada ya kufaulu mtihani wako wa darasa la saba HONGERA SANA.Shule ya Sekondari Ngwilizi ipo umbali wa km.17 kusini-mashariki mwa ofisi za halamashauri ya mji wa Mbinga.Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tar.....Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe.....na mwisho wa kuripoti ni tarehe .....ndani ya siku saba.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

SARE ZA SHULE.

A) WAVULANA WANATAKIWA WAWE NA.

i. Suluari 02 za rangi ya khaki iwe khaki halisi na yenye marinda na mkanda wa staha rangi nyeusi.
ii. Shati 02 za Tetron nyeupe za mikono mifupi kola za kawaida na tai rangi ya khaki.
iii. Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba vinavyomruhusu kutembea haraka au kukimbia.
iv. Soksi rangi nyeusi.
v. Bukta na fulana kwaajili ya michezo:-wavulana rangi nyeusi na wasichana tracksuit rangi nyeusi
vi. Raba kwaajili ya michezo na kazi (Raba nyeusi na soksi za michezo)
vii. Jembe moja (1)lenye mpini na slesha (kwanja) moja (01) kwaajili ya usafi wa mazingira ya shule.
viii. Sweta rangi ya damu ya m zee lenye 'V' shingoni.

B) WASICHANA WANATAKIWA WAWE NA:

i. Sketi 02 rangi ya khaki –mshono uwe wa marinda ya kawaida na zipimwe kiunoni urefu hadi chini ya magoti.**Rinda box hairuhusiwi.**
ii. Mashati 02 mikono mifupi rangi nyeupe tetron na tai rangi ya khaki.
iii. Viatu vyeusi vya kamba –visiwe na kisigino kirefu
iv. Soksi nyeupe pea mbili.
v. Wanafunzi wa dini ya kiislam wanaweza kuvaa suluari ya khaki,short kanzu nyeupe na hijabu nyeupe NB (Suluari iwe pana) na short kanzu iwe pana ivuke magoti.

Vi Wasichana wote watanyoa nywele hawataruhusiwa kusuka.

Vii Sweta damu ya mzee lenye V shingoni.

Viii Jembe 01 lenye mpini na slesha(kwanja) 01 kwaajili ya usafi wa mazingira ya shule.

NB:Vitu hivyo vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni.

MASOMO

Utajifunza masomo yafuatayo:-**URAIA,KIINGEREZA,KEMIA,FIZIKIA,ELIMU YA VIUMBE,HISABATI,KISWAHILI,HISTORIA NA JIOGRAFIA.**

Masomo haya yatafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.Ili masomo haya uyaelewe vizuri huna budi ujibiidishe kuitumia lugha ya kiingereza mara kwa mara uwapo shuleni.

VIFAA KWAAJILI YA MASOMO.

Mwanafunzi anatakiwa awe na

i)Kalamu ya wino na risasi

ii)Mkebe wa hesabu (mathematical set)

iii)Kaunta book quire 3 kumi na mbili (12)kwa kuanzia

iv)Oxford Dictionary ndogo(English to English)

v)Begi dogo la kubebea madaftari (Vifungashio havitaruhusiwa)

MAJUKUMU YA SERIKALI.

Serikali itahudumia uendeshaji wa shule kwa kutoa Ruzuku za uendeshaji pamoja na :-

-Kununua vitabu

-Utoaji wa taaluma na mitihani

-Vitambulisho

-Kugharamia shughuli za michezo

-Kukamilisha ujenzi na kukarabati miundombinu ya shule.

MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI NI KUHAKIKISHA HUDUMA ZIFUATAZO ZINAPATIKANA KWA MWANAFUNZI:-

a) Sare za shule na michezo
b) Vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari na kalamu
c) Chakula kwa wanafunzi wa kutwa na Hostel
d) Matibabu
e) Nauli ya kwenda shule na kurudi kwa wanaotumia usafiri na walioko shule za Sekondari zenye hostel kipindi cha likizo.
f) Mwanafunzi abebe ufagio aina ya chelewa kwaajili ya usafi wa mazingira.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978,na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi ,yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi ,wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuri ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation) kwa wanafunzi watakaokaa hostel.
d) Kutunza usafi wa mwili na mazingiraya shule.
e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

NB:Shule haitamvumilia mwanafunzi ambaye atakiuka kanuni hizo hapo juu.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AKAFUKUZWA SHULE.

1) Wizi
2) Uasherati na ushoga
3) Ubakaji
4) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocain,mirungi,kubeli nk.
5) Kupiga au kupigana
6) Kuharibu kwa maksudi mali ya umma
7) Kudharau Bendera ya Taifa.
8) Kuoa au kuolewa.
9) Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10) Kutoa mimba.
11) Kugoma,kuchochea, na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine.
12) Kukataa adhabu kwa maksudi itolewayo na walimu.
13) Mwanafunzi kumiliki simu ya aina yoyote.

MAMBO MENGINE MUHIMU.

a) Mzazi mara upatapo fomu hii ya kujiunga na kidato cha kwanza unatakiwa kumpeleka mwanao hospitali ya wilaya kwaajili ya kumpima afya.Medical Examination ambayo imejazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi /mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhari soma maelekezo/maagizo haya kwa makini na kuyatekeleza kikamilifu.

MARA ZOTE UKIWA HAPA SHULENI ZINGATIA KUWA ELIMU NI UKOMBOZI.

KARIBU SANA.

.....

G.M. MABENA

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
NGWILIZI SEC. SCHOOL
BOX 152 MBINGA